JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

Simu: +255262963470
Nukushi: +255262963117
Barua pepe: ps@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz

Mji wa Serikali,
Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S. L. P 2996,
**40478 DODOMA**.

## TAARIFA KWA UMMA

## MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA MUHIMU NCHINI KWA MWEZI APRILI 2023

### 1. UTANGULIZI

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Kama tunavyofahamu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inatekeleza jukumu la kufanya tathmini na kuratibu ukusanyaji wa takwimu za mwenendo wa bei za mazao ya chakula na bidhaa muhimu nchini. Kutokana na umuhimu wa taarifa hizi kutumiwa na watoa maamuzi, wazalishaji, wawekezaji, wafanyabiashara na wananchi wote kwa ujumla, Wizara inaendelea kuutaarifu Umma kuhusu tathmini ya bei hizo. Vilevile, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kudhibiti ongezeko la bei za bidhaa muhimu nchini hasa katika kipindi hiki cha Mfungo Mtukufu wa mwezi wa Ramadhani.

### 2. MWENENDO WA BEI ZA MAZAO NA BIDHAA ZA VYAKULA

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

#### i) Mahindi

Bei ya mahindi kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 800 na 1,650 kwa kilo. Bei ya juu ya mahindi imepanda kwa asilimia 1.5 ambayo ni sawa na ongezeko la Shilingi 25 kwa kilo, wakati bei ya chini imepungua kwa asilimia 5.9 sawa na punguzo la Shilingi 50 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi, 2023 ambayo ilikuwa kati ya Shilingi 850 na 1,625 kwa kilo. Bei za chini zipo katika Mikoa ya Ruvuma na Iringa na bei ya juu imeonekana katika Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara.

Uchambuzi unaonesha kuwa wastani wa bei ya mahindi kwa mwezi Aprili 2023 imepungua kwa asilimia 0.8 ukilinganisha na wastani wa bei ya mwezi Machi 2023. Kupungua huko kumesababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini, ambapo kumekuwa na uhakika wa mavuno ya mahindi kwa wakulima wengi, hali ambayo imesababisha wakulima kuachilia akiba waliohifadhi ili kupisha nafasi kwa ajili ya mavuno ambayo yanatarajiwa hivi karibuni. Aidha, kuna taarifa ya mahindi yanayoingia nchini kutoka Zambia na Malawi kwa sababu ya mavuno mazuri katika nchi hizo na kutafuta soko na bei nzuri nchini

Tanzania. Aidha, inazaniwa kuwa wafanyabiashara ambao walikuwa wamehodhi mahindi katika ghala zao wameaanza kuyaachilia sokoni kabla ya kuanza kwa mavuno ya mahindi ya msimu wa kilimo wa 2022/2023 ambao kwa kawaida unambatana na kushuka kwa bei ya zao hilo.

### ii) Unga wa Mahindi

Bei ya Unga wa mahindi kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 1,200 na 2,100 kwa kilo. Bei ya juu ya unga wa mahindi imeshuka kwa asilimia 20.0 sawa na kupungua kwa shilingi 75 kwa kilo, wakati bei ya chini ya unga wa mahindi imeshuka kwa asilimia 20 sawa na kupungua kwa Shilingi 300 ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi 2023 ambayo ilikuwa ni kati ya Shilingi 1,500 na 2,175 kwa kilo. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Iringa, Tabora na Songwe na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Pwani, Lindi, Mara na Dar es Salaam.

Uchambuzi unaonesha kuwa wastani wa bei ya Unga wa Mahindi kwa mwezi Aprili 2023 imepungua kwa kati ya asilimia 2.1 ukilinganisha na wastani wa bei ya mwezi Machi 2023. Upungufu huo wa wastani wa bei umesababishwa na kushuka kwa wastani wa bei ya mahindi ambayo ndiyo malighafi kubwa inayozalisha Unga wa Mahindi.

### iii) Mchele

Bei ya mchele kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 2,350 na 3,500 kwa kilo. Bei ya juu ya mchele imeshuka kwa asilimia 2.8 sawa na pungufu ya shilingi 100 kwa kilo, wakati bei ya chini ya mchele imeshuka kwa asilimia 13 sawa na pungufu ya shilingi 350 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi 2023 ambayo ilikuwa ni kati ya Shilingi 2,700 na 3,600 kwa kilo. Mikoa yenye bei ya chini ni Katavi, Tabora na Mwanza na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Pwani, Kagera na Mtwara.

Uchambuzi unaonesha kuwa wastani wa bei ya mchele kwa mwezi Aprili 2023 imepungua kwa asilimia 2.8 ukilinganisha na wastani wa bei ya mwezi Machi 2023. Sababu kubwa ya kushuka kwa wastani wa bei ya mchele ni hali nzuri ya zao la mpunga katika maeneo mengi yanayozalisha zao hilo nchini kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, hali ambayo imesababisha wakulima kuachilia akiba waliohifadhi ili kupisha nafasi kwa ajili ya mavuno ambayo yanatarajiwa hivi karibuni. Aidha, inazaniwa kuwa wafanyabiashara ambao walikuwa wamehodhi mpunga/mchele katika ghala zao wameaanza kuuachilia sokoni kabla ya kuanza kwa mavuno ya zao la mpunga kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023 ambao kwa kawaida unambatana na kushuka kwa bei ya zao hilo.

### iv) Maharage

Bei ya maharage kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 2,175 na 3,800 kwa kilo. Bei ya juu ya maharage haijabadilika, wakati bei ya chini imeshuka kwa asilimia 27.2 sawa na pungufu ya shilingi 813 ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi 2023 ambayo ilikuwa kati ya Shilingi 2,988 na 3,000 kwa kilo. Bei ya chini inapatikana katika Mikoa ya Ruvuma, Katavi na Songwe na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Manyara, Pwani na Kilimanjaro.

Uchambuzi unaonesha kuwa wastani wa bei ya maharage kwa mwezi Aprili 2023 imepungua kwa asilimia 7.0 ukilinganisha na bei ya wastani ya mwezi Machi 2023. Maharage ni mojawapo ya mazao ambayo yameanza kutoa mavuno na kuingia sokoni na hivyo kusababisha wastani wa bei ya zao hilo kushuka. Aidha, kuna taarifa ya mavuno mazuri ya maharage kwa baadhi ya nchi zinazotuzunguka (Malawi, Burundi na Zambia) na hivyo kupunguza mahitaji ya zao hilo katika soko letu la ndani.

**v) Viazi Mviringo**

Bei ya Viazi Mviringo kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 900 na 1,800 kwa kilo. Bei ya juu imeshuka kwa asilimia 10 sawa na shilingi 200 kwa kilo, wakati bei ya chini imepanda kwa asilimia 1.4 sawa na ongezeko la Shilingi 12 ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi 2023 ambayo ilikuwa kati ya Shilingi 888 na 3,000 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi 2023 ambayo ilikuwa ni kati ya Shilingi 888 na 2,000 kwa kilo. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Singida, Tabora, Geita na Iringa na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Rukwa, Songwe na Pwani.

Uchambuzi unaonesha kuwa wastani wa bei ya Viazi Mviringo kwa mwezi Aprili 2023 imepungua kwa asilimia 2.7 ukilinganisha na wastani wa bei ya mwezi Machi 2023. Kama ilivyo Maharage, Viazi Mviringo ni mojawapo ya mazao ambayo yameanza kutoa mavuno na kuingia sokoni na hivyo kusababisha wastani wa bei ya zao hilo kushuka. Aidha, kuna taarifa ya mavuno mazuri ya Viazi Mviringo kwa baadhi ya nchi zinazotuzunguka (Malawi, Burundi na Zambia) na hivyo kupunguza mahitaji ya zao hilo katika soko letu la ndani.

**vi) Unga wa Ngano**

Bei ya unga wa ngano kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 2,000 na 2,400 kwa kilo. Bei ya juu na ya chini ya unga wa ngano imepanda kwa asilimia 4.3 na 11.1 sawa na ongezeko la Shilingi 100 na 200 kwa kilo mtawalia ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi 2023 ambayo ilikuwani kati ya Shilingi 1,800 na 2,300 kwa kilo. Bei ya chini ipo katika Mikoa tisa (9) nchini na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Songwe, Mbeya na Singida.

Uchambuzi unaonesha kuwa wastani wa bei ya Unga wa Ngano kwa mwezi Aprili 2023 imepungua kwa kati ya asilimia 0.1 ukilinganisha na wastani wa bei ya mwezi Machi 2023. Kushuka kwa wastani wa bei ya Unga wa Ngano kumesababishwa na kushuka kwa jumla kwa wastani wa bei ya mazao ya chakula, hasa ukizingatia kuwa mazao ya chakula yanategemeana na kuingiliana katika matumizi.

**vii) Sukari**

Bei ya sukari kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 2,650 na 3,300 kwa kilo. Bei ya juu ya sukari imepanda kwa asilimia 5.6 sawa na ongezeko la Shilingi 175 kwa kilo, wakati bei ya chini imepungua kwa asilimia1.9 sawa na Shilingi 150 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi ambayo ilikuwa ni kati ya Shilingi 2,700 na 3,125 kwa kilo. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya

Tanga, Singida, Songwe na Manyara na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Ruvuma, Geita, Iringa, Pwani na Rukwa.

### viii) Mafuta ya Kupikia

Bei ya mafuta ya kupikia ya Alizeti kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 4,000 na 8,500 kwa lita. Vile vile, bei ya mafuta ya kupikia ya Mawese (Korie na Safi) ni kati ya Shilingi 3,500 na 7,250 kwa lita. Bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya Alizeti imeshuka kwa asilimia 11.1 sawa na shilingi 500 ikilinganishwa na mwezi Machi, 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 4,500. Vilevile, bei ya chini ya mafuta ya Mawese (korie na safi) imeshuka kwa asilimia 22.2 sawa na Shilingi 1,000 ikilinganishwa na mwezi Machi, 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 4,500 kwa lita. Bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya Alizeti ipo katika Mikoa ya Singida, Iringa na Manyara na bei ya juu ipo katika Mikoa Pwani, Mtwara na Lindi.

Uchambuzi unaonesha kuwa wastani wa bei ya Mafuta ya Kupikia ya Alizeti na Mawese kwa mwezi Aprili 2023 imepungua kwa asilimia 1.7 na 3.4 mtawalia ukilinganisha na wastani wa bei ya mwezi Machi 2023. Kupungua huko kumesababishwa na hali nzuri ya zao la alizeti katika maeneo mengi yanayolima zao hilo nchini kutokana na mvua za wastani zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali, hali ambayo imesababisha wakulima kuachilia akiba waliohifadhi ili kupisha nafasi kwa ajili ya mavuno ambayo yanatarajiwa hivi karibuni. Aidha, wasindikaji wengi wa zao la alizeti wameamua kutumia hifadhi ya alizeti waliyokuwa nayo kwa kuzalisha mafuta zaidi ili kutoa nafasi kwa mavuno yanayotarajiwa kuwa makubwa.

## 3. MWENENDO WA BEI ZA VIFAA VYA UJENZI

### i) Saruji

Bei ya saruji (42.5) kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 14,650 na 24,500 kwa mfuko wa kilo 50. Bei hiyo imeonesha uhimilivu ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi 2023. Mikoa yenye bei ya chini ni Tanga, Dar es Salaam na Mtwara na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Kagera, Kigoma na Mara.

### ii) Nondo

Bei ya nondo mm 10 kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 16,000 na 23,500. Bei ya juu imepanda kwa asilimia 6.8 sawa na shilingi 1,500 ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 22,000. Bei za chini zipo katika Mikoa ya Dodoma, Tanga na Arusha na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Songwe, Ruvuma, Iringa, Manyara na Rukwa.

Bei ya nondo mm 12 kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 22,000 na 28,000. Bei ya chini imepanda kwa asilimia 15.7 sawa na shilingi 3,000 ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 19,000. Bei za chini zipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Singida na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Katavi, Rukwa na Ruvuma.

### iii) Bati

Bei ya bati nyeupe geji 30 kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 21,500 na 30,000. Bei ya juu ya bati imepanda kwa asilimia 9.1 sawa na shilingi 2,500 ikilinganishwa na bei ya mwezi Machi, 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 27,500. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Dodoma, Songwe na Kigoma na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Tabora.

Kwa ujumla, wastani wa bei ya vifaa vya ujenzi (Nondo, Saruji na Mabati) imeendelea kuonesha uhimilivu kwa kutokuwa na mabadilliko ambayo yapo kwenye digiti moja, kitu kinaochoonesha kuhimili mfumoko wa bei. Wastani wa bei ya saruji aina ya 42.5 na ile ya aina ya 32.5 kwa mwezi Aprili 2023 imepungua kwa asilimia 1.1 na 2.0 mtawalia ukilinganisha na wastani wa bei ya saruji ya aina hiyo hiyo kwa mwezi Machi 2023. Hali hii inaweza kuwa imechangiwa na ongezeko la uzalishaji katika viwanda vya ndani vya kuzalisha saruji. Vilevile, wastani wa bei ya mabati ya Geji 32, Geji 30 na Geji 28 kwa mwezi Aprili 2023 imepanda kwa asilimia 2.8, 1.7 na 1.4 mtawalia ukilinganisha na wastani wa bei ya mwezi Machi 2023. Aidha, wastani wa bei ya Nondo za mm 10, mm 12, na mm 16 kwa mwezi Aprili 2023 imepanda kwa asilimia 3.0, 0.8 na 3.0 mtawalia ukilinganisha na wastani wa bei za mwezi Machi 2023. Kupanda kwa bei kwa bidhaa za nondo na mabati kunaweza kuwa kumesababishwa na kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa hizo kwa watumiaji.

## 4. MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA SABUNI

### i) Sabuni

Bei ya Sabuni aina ya Jamaa, White wash na MO kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 2,700 na 3,900 kwa mche. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Kilimanjaro, Shinyanga, Singida, Manyara na Geita na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Mbeya, Kagera, Mara na Katavi.

Bei ya Sabuni aina ya Takasa, kiboko na Kuku kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 1,200 na 4,000 kwa mche. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Geita, Kigoma na Dar es Salaam na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Mbeya, Lindi, Singida na Kagera.

Bei ya Sabuni za Magadi kwa mwezi Aprili ni kati ya Shilingi 1,000 na 3,200. Sabuni za magadi zipo aina mbili nazo ni miche myembamba na miche minene. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Katavi, Kigoma na Morogoro na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Lindi, Singida na Mbeya

## 5. MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA ZA VYAKULA KWA NCHI JIRANI

Kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini na nchi za Jirani, na kuanza kwa mavuno kwa baadhi ya mazao muhimu kama Maharage na viazi mviringo, upatikanaji wa mazao hayo nchini na nchi jirani umeendelea kuongezeka, na hivyo kuchangia kushuka kwa bei za bidhaa za vyakula nchini na nchi jirani.

Aidha, kwa ujumla bei za vyakula katika nchi nyingi duniani zinaendelea kuimarika. Aidha, mfumuko wa bei nchini Tanzania umeendelea kuimarika na kuwa na kiwango cha chini zaidi

ikilinganishwa na nchi jirani, ambapo kwa Tanzania kiwango cha mfumuko wa bei ni asilimia 4.8 kwa mwezi Februari 2023 ikilinganishwa na asilimia 9.2 ya Kiwango cha mfumuko wa bei nchini Kenya, asilimia 9.2 nchini Uganda na asilimia 20.8 nchini Rwanda kwa mwezi Februari, 2023.

## 6. HITIMISHO

**Ndugu Waandishi wa Habari;**
Ukichunguza kwa makini uchambuzi wa mwenendo wa bei za mazao na bidhaa za vyakula zilizowasilishwa, utagundua kuwa zimetumia ulinganisho wa bei ya chini ya mwezi Aprili 2023 na bei ya chini ya mwezi Machi 2023, sambamba na uchambuzi wa ulinganifu wa bei za juu kwa miezi husika. Hata hivyo, ukitumia uchambuzi wa mwenendo wa bei za mazao na bidhaa za chakula kwa kutumia wastani wa bei, uchambuzi unaonesha kwa ujumla wastani bei za mazao yote na bidhaa za chakula zimeshuka kwa asilimia kati 0.8 na 7.0.

Mwisho napenda kutoa majibu juu ya malalamiko ya watuamiaji wa bidhaa ya Saruji aina ya Hauxin inayozalishwa na kiwanda cha Maweni Limestone Limited kilichopo Mkoani Tanga kuhusu upungufu wa uzito wa bidhaa hiyo. Kwa mujibu wa kifungu namba 41(a) na (b) cha Sheria ya Vipimo, Sura ya 340, kinatoa katazo kwa mtu yeyote kuuza bidhaa yoyote iliyo chini ya uzito, kipimo au namba kama inavyohitajika kwa mujibu wa Sheria. Sheria hii pia inatoa katazo kwa mtu yeyote katika ufanyaji biashara kutoa taarifa za uongo juu ya bidhaa yoyote kuhusu uzito, kipimo, namba, geji au kiwango. Endapo makosa haya yatafanyika kwa mtu yeyote wote atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria hii.

Kwa upande wa mwenye duka anajukumu la kuhakiki kila bidhaa anayouza kabla ya kumuuzia mlaji wa mwisho na kujiridhisha kuwa bidhaa husika ipo katika hali inayotakiwa kulingana na matakwa ya Sheria.

Kwa muktadha huo, Sheria hii ya Vipimo sura ya 340 inatoa adhabu mbili kwa mtu ambaye atakuwa ametenda makosa tajwa kama ifuatavyo;

i) Endapo mtu huyu atakuwa amekiri kosa, Sheria inampa mamlaka Kamishna wa Wakala wa Vipimo kufifisha kosa (compounding of offences) na kumtoza faini mtu huyu ya kiasi kisichopungua shilingi laki moja na kisichozidi milioni ishirini, hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 46 cha Sheria ya Vipimo kama kilivyofanyiwa marekebisho na kifungu cha 48 cha Sheria ya marekebisho mbalimbali ya Sheria Na. 3 ya mwaka 2016.

ii) Sheria hii inatoa adhabu ya jumla kwa mtu ambaye atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria hii na ni mkosaji wa mara ya kwanza akitiwa hatiani Mahakamani basi atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki tatu na kisichozidi milioni hamsini au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja, na endapo mtu huyu ni mkosaji wa mara ya pili akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua kiasi cha shilingi laki tano na isiyozidi Milioni mia moja au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 45 cha Sheria ya Vipimo kama kilivyofanyiwa marekebisho na Kifungu cha 47 cha Sheria ya marekebisho mbalimbali ya Sheria Na. 3 ya mwaka 2016.

Baada ya mwenye kiwanda kukiri kosa, atachukuliwa hatua za kisheria kwa kufifilishwa kosa kama ilivyoelezwa hapo juu kwa mujibu wa Sheria ikiwa ni pamoja na kulipa faini na kupewa maelekezo mengine ikiwemo kufanya marekebisho ya mapungufu yaliyojitokeza.

Napenda kutoa rai kwa wazalishaji wa bidhaa zote za viwandani kuongeza jitihada za uzalishaji wa bidhaa kwa ubora unaohitajika sokoni na kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa ili kukabiliana na mfumuko wa bei za bidhaa mbalimbali.



....................................................................

**Exaud Kigahe (Mb)**

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

**13 APRILI, 2023**